

Yusufu wa Arimathaya alikuwa tajiri na alikuwa mfuasi wa Yesu kwa kisiri. Yusufu alienda kwa Pontio Pilato kumuuliza akubali ampe mwili wa Yesu ili aizike. Mwili wa Yesu uliteremshwa kutoka kwa msalaba. Ulfungwa kwa nguo za kitani zilizokuwa na karafuu inukayo vizuri. Uliwekwa kwa kaburi ya Yusufu iliyokuwa kwa bustani yake.

Maswali na Majibu

1. Watu walifanya nini wakipaza sauti Yesu alipoingia Yerusalem? *Waliweka nguo zao barabarani na matawi ya mitende, "Hosana, Mwana wa Daudi. Mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana."*
2. Mkate na divai ilikuwa mfano wa nini? *Mwili wa Yesu unaotolewa kwa ajili yao. Damu ya Yesu imwakikayo kwa ajili yao.*
3. Yuda alifanya nini? *Aliambia Wakuu wa Makuhani penye wanawenza kupata Yesu. Alisaliti Yesu kwa busu.*
4. Petro alifanya nini? *Alikataa kwamba ye ye si mwanafunzi wa Yesu mara tatu.*
5. Kuhani Mkuu alisema eti Yesu alisema nini ya kupata adhabu ya kifo? *Alisema eti ye ye ni Mwana wa Mungu.*
6. Pilato alifanya nini? *Aliosha mikono lakini alihukumu kwamba Yesu auawe.*
7. Mwizi mmoja aliuiliza Yesu afanye nini? *Amkumbuke atakapokuja kusimamisha Ufalme wake.*
8. Nini ilifanya Yesu alipokufa? *Kulikuwa na tetemeko kubwa ya nchi. Pasi ya Hekalu ilipasuka mara mbili.*
9. Mbona askari hawakuvunja miguu ya Yesu? *Kwa sababu alikuwa amekufa.*
10. Yesu alizikwa wapi? *Kwa kaburi ya Yusufu wa Arimathaya.*

Mistari ya kukariri

Wafilipi 2:7 – 8; Warumi 5:8 Yohana 3:16

Mazungumzo

Petro na Yuda walifanya makosa. Yuda alikuwa na hali ya kushtuka namna gani? Alifanya nini? (Mathayo 27:3 – 5). Petro naye alishanka namna gani? (Luka 22:62). Baadaye Petro alikuwa na kazi gani? (2 Petro 1:1). Nasi tunajifunza somo gani kwa hizi hali za kushtuka?

Kuandika

Wakuu wa Makuhani walikuwa wanafanya nini Hekaluni wakati Yesu alikufa? Huu ulikuwa mfano gani yakutuonyesha vile Yesu anatuletea wokovu na msamaha wa dhambi zetu.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

Somo la 36 Kifo cha Yesu



SOMA Marko 11:7 – 11; Marko milango ya 14 na 15


SOMO

Wakati wa juma ya mwisho ya maisha yake, Yesu alienda Yerusalem. Aliuja Mafarisayo na Wakuu wa Makuhani watamsilibisha, lakini alijuwa kwamba hiyo ilikuwa mapenzi ya Mungu. Yesu aliiingia Yerusalem kwa punda. Aliwakuta watu wengi. Walitengeneza zulia ya mitende na mavazi yao ili atembelee. Walipasa sauti, "Hosana, Mwana wa Daudi! Mbarikiwa ndiye Mfalme ajae kwa jina la Bwana!" Watu walitaka Yesu akuwe mfalme wao na awaokoe kutoka kwa Warumi.

Yesu alipoingia Yerusalem akiwa kwa punda, alilia kwa sababu alijuwa kwa muda mchache, watu hawa wenye, watapaza sauti wakisema, asulibishwe. Aliuja Mungu atawaadhibu kwa sababu ya kumuua na atawatawanyisha ulimwenguni kote.

Wakuu wa Makuhani walipanga kuua Yesu. Waliogopa kumshika mbele ya watu aliofuatana nao. Yuda Iskariote alikutana na wakuu wa makuhani na akakubali kumsaliti Yesu kwa fedha 30. Walipanga pamoja vile watamshika Yesu kwa kisiri.

Ilikuwa wakati wa Pasaka, kwa hivyo Yesu na wanafunzi wake walikula chakula cha Pasaka cha kawaida katika chumba kimoja orofani Yerusalem. Hiki chakula cha jioni chenyewe Yesu alishiriki na wanafunzi wake kilikuwa cha maana sana. Yesu alivunja mkate na akawapa kila mmoja wao. Aliwambia kwamba ni ishara ya mwili wake utakaotolewa kwa ajili yao. Halafu akachukua divai na kuipitisha kwa kila mmoja wao. Aliwambia ni ishara ya damu yake itakayomwagwa kwa ajili yao. Yesu aliwambia wawe wakikula mkate na kunywa divai hivyo hivyo kumkumbuka kama dhabihu. Hiki kitendo cha maana kilichoanzishwa na Yesu, kila juma kinatimizwa na Wakristo wa kweli.



Yuda alienda kwa Wakuu wa Makuhani na kuwambia kwamba Yesu atakuwa katika Bustani ya Gethsemane. Pale wangemshika kwa kisiri. Wakuu wa Makuhani wakalipa Yuda vipande 30 vya fedha kumsaliti Yesu.

Baada ya hicho chakula cha jioni, Yesu aliongoza wanafunzi kwenda kwa Bustani ya Gethsemane. Aliomba Mungu ampe nguvu. Aliomba kwa nguvu mpaka akatoa jasho ‘kama matoni ya damu.’ Haikuwa raisi Yesu kufanya mapenzi ya Mungu, lakini kwa sababu alimpenda Mungu sana, alimtii. Kule Yuda alikuja na askari na makuhani. Yuda alimbusu Yesu kuwaonyesha askari ni huyo wa kushika. Yesu alienda nao bila kushindana. Wanafunzi wote walitoroka isipokuwa Petro na Yohana waliofua Yesu nyuma lakini kwa umbali.

Wakati wa chakula cha jioni Yesu aliambia Petro kwamba atamkana mara tatu kabla jogoo irike. Lakini Petro hakumwamini. Ndani ya ua ya Kuhani Mkuu, Petro aliulizwa mara tatu kama yeye ni mwanafunzi wa Yesu. Kila alipoulizwa alikana. Baada ya mara ya tatu, jogoo iliwiha halafu Yesu akageuka na kuangalia Petro. Petro alikumbuka akaenda inje na kulia kwa uchungu.

Kuhani Mkuu aliita mashaidi wengi wa uongo, lakini haikukubalika. Kwa desturi ya sheria, Yesu angeachiliwa. Lakini Kuhani Mkuu alikuwa ameamua Yesu afe. Yesu alipokubali kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, hiyo ilikuwa sababu ya kusema amekufuru - alizungumza kinyume. Kulingana na sheria za Kiyahudi, kukufuru, adhabu yake ni kifo. Ingawaje Yesu hakukuwa amekufuru Mungu. Alikuwa anasema ukweli. Lakini Kuhani Mkuu akasema lazima Yesu auawe. Alipeleka Yesu kwa Pontio Pilato, Gavana wa Warumi, kwa sababu Pilato tu ndiye angearisha hukumu ya kifo.



Baada ya Pilato kumhoji Yesu, aliona kwamba hakukuwa na hatia. Tena alikundua kuwa makuhani ni adui wa Yesu na walitaka auawe. Pilato alitaka amwaachilia Yesu. Lakini Wakuu wa Makuhani na watu walipiga kelele na kusema, “Msulibishe! Msulibishe! Hatimae Pilato alikubali kwamba Yesu asulibishwe. Aliosha mikono yake mbele ya Wayahudi kuwaonyesha kwamba yeye hana hatia kwa kifo cha Yesu. Alisema, “Sina hatia kwa damu ya huyu mtu.” Wayahudi walijibu, “Wacha damu yake iwe kwetu na kwa watoto wetu.” Hii ilikuja kuwa kweli kwa sababu Mungu aliadhibu Wayahudi. Baada ya miaka 40, Warumi waliharibu Yerusalem na Wayahudi walitawanyika ulimwengu mzima.

Askari wa Warumi walivaa Yesu joho ya zambarau na taji ya miiba kichwani. Walimdhihaki kwa kumwita Mfalme wa Wayahudi. Walimtemea mate na kumpiga.

Wafungwa walibeba misalaba yao wenyewe wakienda penye watasulibiwa. Yesu alikuwa amechoka sana kutokana na kupigwa. Alikuwa ametokwa na damu nyingi. Hangeweza kubeba msalaba peke yake. Askari wa Warumi walilazimisha mtu aliyejikuwa anasafiri kwa hiyo barabara kubeba msalaba na Yesu.

Kusulibiwa ilikuwa njia katili na mbaya sana ya kuua mtu. Mikono na miguu ya mahabusi iligongewa na misumari kwa msalaba na kukaa kule mpaka wafe. Askari walipokuwa wakimgongea msalabani, aliomba na kusema, “Baba, wasamehe, hawajui wafanyalo.” Askari hawakujua kwamba jambo walilokuwa wakifanya ni mbaya sana, kusulibisha Mwana wa Mungu.

Wezi wawili walisulibiwa na Yesu. Wale wezi walimlaani Yesu. Lakini baadaye mmoja wao alisema, “Sisi ni waalifu. Tunastahili kuadhibiwa. Lakini mtu huyu hajafanya kosa lolote.” Halafu aksauliza Yesu amkumbuke atakapokuja kusimamisha Ufalme wake. Yesu alimwaahidi kwamba atakuwa kwa Ufalme.

Yesu aliona kikundi cha watu wamesimama karibu. Kati yao kulikuwa na mama yake na Yohana mwanafunzi wake. Yesu aliambia Yohana kumlinda mama yake na Mariamu amchukue Yohana kama mwanawe.

Umati wa watu walimfanya mzaha na kumdhihaki Yesu. Watawala walipiga kelele wakisema kwamba kama angekuwa Mwana wa Mungu ashuke chini kutoka msalabani. Kwa masaa matatu juu halikuwaka na giza ilitanda dunia mzima. Yesu alipokuwa akikufa, aliita Mungu, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Lakini Yesu aliweka imani yake na akaiweka uhai wake mikonono mwa Mungu. Yesu alipokufa, kulikuwa na mtetemeko wa nchi na pasia ya Hekalu iliraruka kutoka juu mpaka chini ikawa vipande viwili.

Wakati Yesu alikufa, makuhani walikuwa wanachinja mwana kondoo wa chakula cha Pasaka. Wakati wa Musa, damu ya mwana kondoo wa Pasaka iliokea Waisraeli kutoka kwa kifo. Yesu ni kama mwana kondoo wetu wa Pasaka. Damu yake iliyomwagika kwa msalaba inatupa msamaha wa dhambi na tumaini la uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu hapa duniani.

Watawala wa Wayahudi walilizila Pilato ahakikishe kwamba watu waliosulibiwa wamekufa kabla ya Pasaka kuanza. Pilato alituma askari wahakikishe kwamba wamekufa. Askari walifunja miguu ya wale wezi ili wakufe haraka. Lakini Yesu alikuwa amekufa zamani kwa hivyo miguu yake haikuvunjwa. Askari mmoja alimchoma mkuki kwa ubavu kuhakikisha kwamba amekufa.

